DARASA NDANI YA MADHABAHU YA MAARIFA YA NENO LA MUNGU

# YATAMBUE MAENEO 3 AMBAYO KILA NENO UNALOONGEA UNALIANDIKA HAPO KUHUSU MAISHA YAKO

Mwl. Samuel Kibiriti

**Mwalimu Samwel Kibiriti**.

Mawasiliano;

Simu: +255 765 867 574
+255 785 855 785
+255 673 784 197
Baruapepe:pastorkibiriti@gmail.com

Toleo la kwanza 2024

Nunua nakala halisi ili kuinua huduma hii.

**Haki Zote Zimehifadhiwa**,
Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kudurufu, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki au sehemu yake yoyote kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya maandishi toka kwa mwaandishi wa kitabu hiki.

**Kimesanifiwa na**

Truth Printing
0764 425 704/ 0692 637 282
geofreymakula@gmail.com
Dar es Salaam-Tanzania

Bwana Yesu Kristo atukuzwe, mwana wa Mungu karibu katika darasa letu ndani ya Madhabahu ya Maarifa ya Neno la Mungu ili tuweze kujifunza Neno la Mungu na kupokea maarifa na Ufahamu unaotoka ndani ya Neno la Mungu. Ndani ya moyo wangu naongozwa niweze kushirikiana nawe ujumbe huu wa Neno la Mungu ambao utakujenga na kukuimarisha pia kukufungua na kukuweka huru kumbuka Biblia inasema kwamba **"Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, Akawaponya na shida zao. Hulituma neno lake, huwaponya, Huwatoa katika maangamizo yao"** ( Zaburi 107:19-20 ) kanuni kuu ya Mungu unapomlilia kutokana na hali unazopitia kimaisha anachofanya ni kukutumia Neno lake ambalo ndani ya hilo Neno kuna msaada wako na kuna majibu ya kilio chako ambacho ulimlilia.

Kila mwanadamu aliyepo hapa duniani anao ulimwengu wake wa roho ambao ndio umebeba maisha yake yote ya kimwili na ulimwengu wako wa roho umebeba mambo mengi sana kuna masomo nitayaandaa ambayo nitakufunulia vitu

mbalimbali vilivyomo kwenye ulimwengu wako wa roho, ila hapa nataka utambue kwamba kwenye ulimwengu wako wa roho maneno unayoongea kila siku na maneno unayotamkiwa kila siku yanahusika sana na hali ya ulimwengu wako wa roho inategemea kila siku unaongea maneno gani na kila siku unatamkiwa maneno gani. Katika Darasa hili natamani niseme nawe mambo kadhaa kuhusu mahusiano ya ulimwengu wako roho na maneno ya kinywa chako kwa sababu kila siku tokea ukiamka kitandani kuna maneno mengi huwa unaongea na kuyazungumza yanayohusiana na maisha yako unayoishi.

Mtumishi wa Mungu Ayubu alisemaga hivi **"Laiti maneno yangu yangeandikwa sasa! Laiti yangeandikwa kitabuni! Yakachorwa katika mwamba milele, Kwa kalamu ya chuma na risasi"** ( Ayubu 19:23-24 ). Katika tafsiri ya Neno Biblia inasema kwamba **"Laiti maneno yangu yangewekwa kwenye kumbukumbu, laiti kwamba yangeandikwa kwenye kitabu, kwamba yangechorwa kwenye risasi kwa kifaa cha chuma, au kuyachonga juu ya mwamba milele!"**. Unaona Ayubu anaweka wazi

kwamba maneno yake ambaye ameyaongea ingefaa yaandikwe na kuwekwa kuwa kumbukumbu hii inatufundisha kwamba maneno ambayo mwanadamu anayaongea yanaandikwa na kuwa kumbukumbu kwenye ulimwengu wa roho.

Kwahiyo usipende tu kuongea kila neno unalojisikia kuongea elewa kwamba hayo maneno yote unayoongea unayaandika kwenye ulimwengu wako wa roho lakini pia kuna maeneo ambayo iwe unajua au haujui unayaandika maneno yako huko kwenye hayo maeneo ambayo nitakufundisha ndani ya Darasa hili la Maarifa. Nataka ujiulize katika ulimwengu wako wa roho kuna kumbukumbu za maneno gani uliyoyaandika kwa kinywa chako?. Malaika wa Mungu Gabriel alipoenda kwa Danieli alimwambia hivi **"Akaniambia, Ee Danielii, mtu upendwaye sana, yafahamu maneno nikuambiayo, ukasimame kiwima-wima; maana kwako nimetumwa sasa. Na aliponiambia neno hili, nalisimama nikitetemeka. Ndipo akaniambia, Usiogope, Danielii; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako,**

**maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako"** ( Danieli 10:11-12 ).

Malaika anamwambia wazi Danieli kuwa maneno yake aliyoongea akiwa duniani kwenye ulimwengu wa roho yalisikiwa na Mungu alipomaliza kuyasikiliza akamtuma malaika wake kwenda kwenye maisha ya Danieli. Tafsiri ya Neno Biblia inaweka vizuri kwamba **"Akasema, Danieli, wewe mtu upendwaye sana, fikiri kwa makini maneno ninayokwenda kunena nawe sasa; simama wima, kwa maana sasa nimetumwa kwako. Naye aliponiambia haya, nikasimama nikitetemeka. Ndipo akaendelea kusema, Danieli, usiogope. Tangu siku ya kwanza ulipotia moyo wako ili kupata ufahamu na kujinyenyekeza mbele ya Mungu wako, maneno yako yalisikiwa, nami nimekuja ili kujibu maneno yako"**. Malaika wa Mungu anamwambia Danieli amekuja ili kujibu maneno yake, je! Wewe kupitia maneno unayoongea kila siku yakisikiwa kwenye ulimwengu wa roho wanatumwa viumbe kutoka upande gani kuja kujibu maneno yako? Wanatumwa viumbe kutoka Ufalme wa Mungu au ufalme wa shetani?

Kuwa mwangalifu sana na maneno unayoongea kila siku kuhusu maisha yako.

Waebrania 11:3 Biblia inasema kwamba **"Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri"** ( Waebrania 11:3 ). Mungu alipokuwa anaumba ulimwengu alitumia maneno ya kinywa chake katika kutamka na kila neno alilotamka lilitendewa kazi na Roho wake na likaonekana kwenye uhalisia wake hii inatufundisha kwamba na sisi kwa maneno ya vinywa vyetu tunaweza kuumba mambo mazuri au mambo mabaya ndio maana tunahitajika sana kuwa waangalifu kwenye maneno ya vinywa vyetu tunayoongea kila siku kuhusu maeneo mbalimbali ya maisha yetu bila kujalisha tunapitia wakati gani wa kimaisha tunatakiwa kuchunga sana maneno yetu.

Nataka ufahamu kwamba Mungu anacho kinywa ambacho amekitumia na anakitumia kuongea maneno **"Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"** ( Mathayo

4:4 ) na Mungu katika uumbaji wake katika kitabu cha Mwanzo sura yote ya kwanza tumeona jinsi alivyokitumia kinywa chake kuumba na kutamka maneno yaliyengeneza mbingu na nchi. Pia Mungu amempatia mwanadamu kinywa **"Bwana akamwambia, Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu?...."** ( Kutoka 4:11 ) na Mungu kutupatia wanadamu kinywa alitegemea kuona maneno mazuri yanatoka kwenye vivywa vyetu sio maneno mabaya naya uovu, kwahiyo mimi na wewe tuweze kubadilika sasa na kutumia kinywa kutamka maneno mazuri ambayo yatatengeneza maisha yetu kuwa bora naya thamani hapa duniani.

Biblia inasema hivi **"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru"** ( Mwanzo 1:1-3 ). Mungu alisema kwa kinywa chake kwamba iwepo nuru na nuru ikatokea kwahiyo tunajifunza kuna nguvu kubwa sana ya kiroho katika maneno lakini sisi je! Tunaongea maneno gani kuhusu maisha yetu na hali tunazopitia kimaisha?.

### **( a ) Katikati ya ukiwa Mungu kwa maneno yake aliandika Nuru**.

Mungu aliona kabisa kuna ukiwa ambao umefunika duniani na alichokifanya alisema iwe nuru kwenye hali hiyo ya ukiwa na Biblia inasema lile neno iwe nuru likatengeneza nuru kwenye mazingira ya ukiwa na nuru ikaonekana. Unapopita katika maisha kwenye mazingira ya ukiwa hutakiwi kuongea maneno mabaya au kuongea maneno yasiyofaa bali tujifunze hapa kwa Mungu kwamba tukikutana na mazingira ya ukiwa maishani mwetu tutumie vinywa vyetu vizuri kwa kutamka neno kwamba kwenye huu ukiwa natangaza iwe nuru kwa Jina la Yesu Kristo na hilo neno litatengeneza na kusababisha nuru itokee kwenye hiyo hali ya ukiwa.

### **( b ) Katikati ya utupu Mungu kwa maneno yake aliandika Nuru**.

Katika uumbaji wa Mungu alikutana na mazingira ya duniani katika hali ya utupu lakini Mungu alitumia kinywa chake kutamka nuru na baada ya Mungu kusema neno nuru tunaona kwamba nuru ikajitokeza kwenye utupu uliokuwepo kwenye uso

wa duniani. Hii inatufundisha kwamba tukipitia hali ya kimaisha ya utupu tunachotakiwa ni kutamka nuru kwa maneno yetu kwenye hali hiyo na neno hilo nuru litaotengeneza nuru kuonekana kwenye hali ya utupu.

### ( c ) Katikati ya giza Mungu kwa maneno yake aliandika Nuru.

Mungu kwenye uumbaji wake katika ulimwengu alikutana na mazingira ya giza ambalo lilikuwa limetanda na Mungu alichofanya hakushindana na giza wala kulikemea bali alitumia kinywa chake kutamka Nuru katikati ya mazingira ya giza na ile nuru ikaonekana na Mungu kuifurahia. Hapa tunapata somo kwamba kwenye vipindi vya maisha yetu hapa duniani tutakutana na mazingira ya giza na hali hizo zikija maishani mwetu hatutakiwi kulia na kulalamika bali tunatakiwa kutumia vinywa vyetu na kutamka neno kwamba kwenye mazingira haya ya giza katika maisha yangu natamka iwe nuru kwa Jina la Yesu Kristo kisha utaiona nuru ya Mungu ikichomoza kwenye giza ambalo lilikuwa linakutisha.

Mungu alitumia vyema kinywa chake kutamka maneno na sisi ni mfano na sura ya Mungu **"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi"** ( Mwanzo 1:26 ) kwahiyo mazingira ya aina yoyote tutakayokutana nayo kimaisha au hali tofauti tofauti tunazopitia leo maishani mwetu tunatakiwa kutumia vizuri vinywa vyetu kwa kutamka maneno ambayo yatapindua na kugeuza na kubadilisha hali tunazoziona na kuzipitia na hilo linawezekana kama tutaacha kuongea maneno ya upuuzi na ujinga na uovu kwenye vinywa vyetu.

● Baada ya kujifunza hapa kwenye mfano huu wa Mungu alivyotumia kinywa chake kutamka maneno nataka tusongee ndani kidogo ambapo nataka nikuonyeshe maeneo ambayo umeandika maneno yako mwenyewe yale ambayo unayaongea sasa ujichunguze kwamba ni maneno ya aina gani umeandika hapo? Kama utagundua sio maneno mazuri uliyoandika kupitia kinywa chako ingia kwenye maombi tumia Damu ya Yesu Kristo

kuyafuta hayo maneno pia tumia Jina la Yesu Kristo kuyaondoka hayo maneno ili yasitende kazi wala kutumiwa na maadui kukufunga na kukutesa kimaisha.

## TAFAKARI MISTARI HII YA BIBLIA KUHUSU MANENO KWENYE KINYWA CHAKO.

Mungu amekupatia kinywa sio ukitumie kuongea kila neno kuhusu maisha au au kuongea kila neno kuhusu hali yako unayopitia kimaisha pia Mungu hajakupa kinywa chako kuongea kila neno ambalo umelisikia kutoka kwa wanadamu wanaokuzunguka au umelisikia kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya habari au kwenye mitandao ya kijamii bali Mungu amekupatia kinywa uweze kukitumia kuongea maneno mazuri ambayo yatabadilisha hali zako mbaya unazopitia maishani mwako pia utumie kinywa chako kuongea maneno ambayo yatakupatia kesho njema ya hatima yako ya maisha. Neno la Mungu linasema **"Maneno ya kinywa changu, Na mawazo ya moyo wangu, Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu, na mwokozi wangu"**

( Zaburi 19:14 ) maneno ya kinywa chako yanatakiwa kupata kibali mbele za Mungu kwa maana kuwa unatakiwa kuongea kwenye kinywa chako maneno mazuri yenye utukufu kwa Mungu ndipo yatapata kibali mbele za Mungu ila ukiongea maneno hovyo hayatapata kibali mbele za Mungu.

Mungu alimwambia Musa awaambie wana wa Israeli kwamba **"Waambieni, Kama niishivyo, asema Bwana, hakika yangu kama ninyi mlivyonena masikioni mwangu, ndivyo nitakavyowafanyia ninyi"** ( Hesabu 14:28 ). Mungu anasikiliza maneno tunayoongea kupitia vinywa vyetu swali ni hili Mungu anapotega sikio lake maishani mwako anakusikia unaongea maneno ya aina gani? Maneno ya baraka au laana? Maneno ya hekima au ya upumbavu? Ni lazima tuchunge sana maneno ambayo tunayaongea kwa sababu kwenye ulimwengu wa roho yanasikilizwa na tutafanyiwa sawasawa na hayo maneno tulioongea.

Biblia inasema kwamba **"Kinywa chake kimejaa laana, Na hila na dhuluma. Chini ya ulimi wake kuna madhara na uovu"** ( Zaburi 10:7 ). Maana yake ni kwamba maneno anayotoa kwenye

kinywa chake ni maneno ya laana tu, je! Wewe kwenye kinywa chako unatoka maneno ya baraka au ya laana? Kama unatoa maneno ya laana badilika kuanzia sasa kwasababu unaharibu mwenyewe maisha yako na anza kuongea maneno ya baraka kupitia kinywa chako.

Biblia inasema **"Maneno ya kinywa chake ni uovu na hila, Ameacha kuwa na akili na kutenda mema"** ( Zaburi 36:3 ). Maneno ya kinywa kuwa uovu maana yake ni kuongea maneno ya upuuzi na ujinga ndio maana Biblia inasema uovu, je! Wewe kwa kinywa chako huongei maneno ya upuuzi na ujinga? Kama unaongea hayo maana yake Mungu akikiangalia kinywa chako anakiita cha uovu kwahiyo badilika kuanza sasa na usitamani kinywa chako kuwa cha uovu kutokana na maneno unayojitamkia kila siku.

Biblia inasema **"Kinywa chake mwenye haki hunena hekima, Na ulimi wake husema hukumu"** ( Zaburi 37:30 ). Kinywa cha mwenye haki kinaongea maneno ya hekima ila kinywa cha mjinga kinaongea maneno ya upumbavu kwahiyo tamani kinywa chako kiwe chenye haki kwa

kutamka maneno ya hekima kila siku maishani mwako.

Biblia inasema **"Umekiachia kinywa chako kinene mabaya, Na ulimi wako watunga hila"** ( Zaburi 50:19 ). Kinywa chako usikiachie kunena mabaya bali kinywa chako kiachie kinene maneno mema kwaajili ya maisha yako pia kinene maneno mema kwaajili ya familia yako na uzao wako pia kiachie kinywa chako kinene maneno mema kwaajili ya wanadamu wanaokuzunguka.

Biblia inasema **"Ambazo midomo yangu ilizinena; Kinywa changu kikazisema nilipokuwa taabuni"** ( Zaburi 66:14 ). Unapokuwa kwenye maisha ya taabu na shida au unapopita nyakati ngumu kimaisha unakitumia kinywa chako kuongea maneno gani? Hakikisha hata ukiwa taabuni usikiruhusu kinywa chako kuongea maneno ya makufuru mbele za Mungu **"Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru..... "** ( Ufunuo wa Yohana 13:5 ). Maneno makufuru ni maneno yasiyokuwa na utukufu mbele za Mungu ni maneno ya kuishusha chini hadhi na heshima na ukuu wa Mungu kwahiyo usikubali kabisa Shetani akitumie

kinywa chako ukiwa kwenye wakati wa taabu kimaisha uongee maneno ya makufuru kumhusu Mungu usijaribu kufanya hilo.

Biblia inasema **"Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu"** ( 2 Timotheo 2:16 ). Mungu anakusihi sana kupitia Neno lake ujiepushe kabisa mbali na maneno yasiyofaa kuwahiyo usijaribu kabisa kutumia kinywa chako kuongea au kutamka maneno yasiyofaa kuhusu maisha yako au kuhusu familia na uzao wako au kuhusu wanadamu wengine au kuhusu nchi yenu na taifa lenu bali kitumie kinywa chako kwaajili ya kuongea maneno yanayofaa.

Biblia inasema **"Basi umetegwa kwa maneno ya kinywa chako, Umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako"** ( Mithali 6:2 ). Maneno unayoongea kupitia kinywa chako yanaweza kukufanya uwe huru au ufungwe na kuteswa kwahiyo hakikisha kwamba unakitumia vizuri kinywa chako kuongea maneno mazuri naya baraka ili usijiingize kwenye mitego.

Biblia inasema **"Maana kinywa changu kitasema kweli, Na uovu ni chukizo kwa midomo yangu"** ( Mithali 8:7 ). Hakikisha unakitumia kinywa chako kusema kweli maana yake maneno yanayotoka kwenye kinywa chako yasiwe ya uongo bali yawe ya kweli bila kujalisha mazingira yakoje, hata kama mazingira yanakulazimisha utumikie kinywa chako kuongea maneno ya uongo usikubali kabisa bali sema kweli kwa kinywa chako nawe utakuwa Baraka kwa Mungu kuliko kusema uongo upate vitu fulani lakini mbele za Mungu ukawa chukizo na laana.

Biblia inasema **"Hufumbua kinywa chake kwa hekima, Na sheria ya wema i katika ulimi wake"** ( Mithali 31:26 ). Hakikisha kila muda ukitaka kufungua kinywa chako kuongea uweze kuongea maneno ya hekima na maneno ya baraka na maneno mema lakini kama unataka kufumbua kinywa chako kuongea maneno ya upuuzi na ujinga ni heri ukaendelea kufunga kinywa chako wala usikifumbue kabisa utakuwa mwenye hakima mbele za Mungu kukizuia kinywa chako kuongea maneno ya upuuzi na ujinga.

Biblia inasema **"Kinywa chake kimejaa maneno matamu, Ndiye mzuri sana pia pia. Ni huyu mpendwa wangu, ni huyu rafiki yangu, Enyi binti za Yerusalemu"** ( Wimbo Ulio Bora 5:16 ). Je! Wewe kinywa chako kimejaa maneno gani matamu au machungu? Hakikisha kwamba kila siku Mungu anayokupa ya kuishi hapa duniani kinywa chako kinajaa maneno matamu ambayo unayaongea na kuyatoa hakika utakuwa ni tunu ya Mungu mwenye ulimwengu huu.

Biblia inasema **"Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo"** ( Ufunuo wa Yohana 16:13 ). Usikubali na kuruhusu kinywa chako kitoe roho chafu ambazo zinatokana na maneno unayoongea kupitia kinywa chako kila siku bali hakikisha kinywa chako kinatoa roho nzuri sababu ya maneno mazuri unayoongea kila siku. Namaanisha kwamba ukisema maneno ya matusi maana yake hayo maneno yanaambatana na roho chafu za matusi bali usikisema maneno mazuri ya baraka hayo maneno yanaambatana na roho nzuri.

**KWA MANENO YAKO UNAWEZA KUANDIKA KATIKA MAENEO HAYA YAFUATAYO**:

Nataka nikuonyeshe angalau maeneo 3 ambayo unayatumia kila siku ya maisha yako kuandika maneno yanayotoka kwenye kinywa chako na maeneo haya yamebeba pia hatima ya maisha yako hapa dunia hivyo unatakiwa kuwa mwangalifu sana kuanzia leo kuchunga maneno unayoyatoa kwenye kinywa chako kwa sababu unakuwa unayaandika kwenye maeneo haya yasiyopungua matatu ninayoenda kukuonyesha hapa.

ENEO LA KWANZA:

**Kila neno unaloongea kwa kinywa chako unaliandika kwenye ulimwengu wa roho wa maisha yako**.

Fahamu wazi kwamba kila neno ambalo unaongea kwa kinywa chako/mdomo wako unaliandika kwenye ulimwengu wa roho wa maisha yako na hilo neno litasimama maishani mwako na kutenda kazi kwa sababu umeshaliandika mwenyewe kwenye ulimwengu wako wa roho, pia fahamu maneno yote ambayo wanadamu wanakutamkia kila wakati yanaandikwa kwenye ulimwengu wako wa roho wa maisha ndio maana unatakiwa kujifunza hili hakikisha unaambatana na marafiki na watu ambao wanakutamkia maneno mazuri ya baraka ni hatari kuwa na marafiki au kuambatana na watu wanaokutamkia maneno ya laana. Hakikisha unaongea maneno yenye utukufu kuhusu maisha yako ya kila siku hapa duniani bila kuangalia unapitia vipindi gani vya kimaisha iwe unapitia wakati wa amani au vita iwe unapitia wakati wa furaha au kilio wewe hakikisha unatumia kinywa

chako kuongea maneno mazuri sababu hayo maneno unayaandika kwenye ulimwengu wako wa roho wa maisha.

Katika maisha yako kabla hujamlaumu Shetani nankugombana naye ujichunguze wewe mwenyewe kwa sababu Shetani hawezi kudhuru maisha yako ni mpaka wewe mwenyewe uweze kumpatia uhalali au nafasi **"wala msimpe Ibilisi nafasi"** ( Waefeso 4:27 ). Unaweza kumpata Shetani nafasi kwenye maisha yako kutokana na maneno unayoongea kila siku tokea unapoamka kitandani hadi unapolala pia unaweza kumpatia shetani nafasi kutokana na mawazo yako machafu unayowaza au kutokana na mwenendo na tabia yako mbaya au kutokana na dhambi unazofanya na kumbuka hili nafasi yoyote unayompatia Shetani kwenye maisha yako ataitumia kuharibu maisha yako au kufunga maisha yako au kuteka vitu vyako vya thamani vya maisha yako ataviiba ndio maana Mungu ametuasa kwamba tusikubali kabisa kumpatia nafasi Shetani kwenye maisha yetu.

Maisha unayoyaishi sasa hivi chanzo ni wewe mwenyewe kutokana na maneno ambayo umeyaandika kwenye ulimwengu wako wa roho

hivyo unatakiwa kufanya tathimini ulianguka wapi? **"Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu"** ( Ufunuo wa Yohana 2:5 ). Jichunguze unaongea maneno gani kupitia kinywa chako kabla ya kuwalaumu wanadamu wengine, sababu Shetani na kuzimu na maadui wameyatumia maneno yako uliyoyaandika kwenye ulimwengu wako wa roho kuyatekeleza ili yawe kama ulivyoongea.

- Kwa mfano kama umeongea kwa kinywa chako maneno kwamba wewe ni maskini maana yake kwenye ulimwengu wako wa roho umejiandikia mwenyewe kwamba wewe ni maskini hivyo Shetani na kuzimu wako kwenye maisha yako kutimiza hayo maneno na kuhakikisha unaishi kama maskini sio tajiri.

- Kwa mfano kama umeongea kwa kinywa chako maneno kwamba wewe niwa kuteseka na kuumwa maana yake kwenye ulimwengu wa roho wa maisha yako umejiandikia mwenyewe kwamba wewe niwa mateso pia ni magonjwa tu hivyo

Shetani na kuzimu wako kwenye maisha yako kuyatimiza hayo maneno yako uliyoyaandika na kuhakikisha unaishi kwenye mateso na magonjwa badala ya kuishi kwenye afya njema na uzima na kuishi kwa furaha na amani.

Kila neno unalolisema na kulitamka kwenye kinywa chako ufahamu kwamba unaliandika mwenyewe kwenye ulimwengu wako wa roho wa maisha na Mungu au Shetani pia Malaika au mapepo watakuja maishani mwako kutimiza hilo neno na kukufanya unaishi kama ulivyosema. Ukiongea maneno ya Baraka na yaliyo na utukufu wa Mungu ujue Mungu na malaika zake na Roho Mtakatifu na Yesu Kristo watayatimiza maishani mwako lakini ukiongea maneno ya uovu na mabaya ujue Shetani na mapepo na miungu watayatimiza maishani mwako.

Wewe ndiye unayeweza kuufanya ulimwengu wako wa roho wa maisha uwe wa Baraka na kuwa huru au ulimwengu wako wa roho wa maisha uwe wa laana na uliofungwa kutokana na maneno unayoongea ndani ya siku nzima Mungu anayokupatia kuishi hakikisha unaufanya kila siku ulimwengu wako wa roho uwe ni sehemu ya

Baraka na utukufu wa Mungu tu na utayaona matendo makubwa ya Mungu maishani mwako hapa duniani kila siku.

## ( 1 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Baraka zako za maisha.

Fahamu kwamba ulimwengu wako wa roho unahusika na Baraka zako za maisha ambazo unatakiwa kuwa nazo kila siku hapa duniani **"Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo"** ( Waefeso 1:3 ). Kwahiyo kwa maneno yako unayoongea kila siku kwa kinywa chako yanaweza kuzuia na kufunga baraka zako zisije maishani mwako ndio maana hakikisha kila siku kwa kinywa chako unaongea maneno mazuri na kuzikiri ahadi za Mungu zilizomo ndani ya Neno lake kuhusu maisha yako.

Mungu alimwambia Haruni kama kuhani kwamba **"Kisha Bwana akanena na Musa, na kumwambia, Nena na Haruni na wanawe, uwaambie, Hivi ndivyo mtakavyowabarikia wana wa Israeli; mtawaambia; Bwana**

**akubarikie, na kukulinda; Bwana akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili; Bwana akuinulie uso wake, na kukupa amani. Ndivyo watakavyoweka jina langu juu ya wana wa Israeli; nami nitawabarikia"** ( Hesabu 6:22-27 ).

Mungu alitaka Haruni kama kuhani watumie vinywa vyao kutamka maneno ya baraka kwenye maisha ya wana wa Israeli na hayo maneno yataandikwa kwenye ulimwengu wao wa kiroho, ndivyo na wewe ninavyotaka ufahamu kwamba kwenye ulimwengu wako wa roho unaweza kuandika maneno ya baraka kama utatumia kinywa chako kuongea baraka lakini ukitumia kinywa chako kuongea maneno ya laana hayo maneno ujue kwamba mwenyewe unayaandika kwenye ulimwengu wako wa roho kwamba wewe ni mlaaniwa badala ya kuwa mbarikiwa.

**TAMKA MANENO HAYA YA BARAKA MAISHANI MWAKO KILA SIKU KWA KINYWA CHAKO**:

Biblia inasema kwamba **"Atapokea baraka kwa Bwana, Na haki kwa Mungu wa wokovu wake"** ( Zaburi 24:5 ). Tumia kinywa chako kutamka maneno haya kila siku kwamba **Mimi nimepokea baraka kutoka kwa Bwana Mungu wangu kwaajili ya maisha yangu Kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema **"Baraka humkalia mwenye haki kichwani; Bali jeuri hufunika kinywa chake mtu mwovu"** ( Mithali 10:6 ). Tumia kinywa chako kutamka maneno haya kila siku kwamba **Baraka za Mungu zimekaa juu ya kichwa changu mimi mwenye haki kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema **"Baraka ya Bwana hutajirisha, Wala hachanganyi huzuni nayo"** ( Mithali 10:22 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Baraka za Mungu zimenitajirisha maishani mwangu nami**

**nitaishi maisha ya utajiri kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Mtu mwaminifu atakuwa na baraka tele; Lakini afanyaye haraka kuwa tajiri hakosi ataadhibiwa"** ( Mithali 28:20 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Mimi ni mtu mwaminifu kwahiyo nitakuwa na baraka tele za Mungu wangu katika maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani"** ( Wagalatia 3:14 ). Tamka kwa kinywa chako maneno haya kwamba **Mimi nipo ndani ya Yesu Kristo kwahiyo baraka za Ibarahimu zinatenda kazi maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Bali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo"** ( Kumbukumbu la Torati 8:18 ). Tamka kwa

kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Mungu naomba unipe nguvu za kupata utajiri maishani mwangu kwasababu niko ndani ya agano la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Bwana hufukarisha mtu, naye hutajirisha; Hushusha chini, tena huinua juu"** ( 1 Samweli 2:7 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Mungu Baba asante kwa kunitajirisha kwa baraka zako maishani mwangu pia asante Mungu Baba kuniinua juu kimaisha hapa duniani kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Utajiri na heshima hutoka kwako wewe, nawe watawala juu ya vyote; na mkononi mwako mna uweza na nguvu; tena mkononi mwako mna kuwatukuza na kuwawezesha wote"** ( 1 Mambo ya Nyakati 29:12 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Mungu Baba umeyafanya maisha yangu hapa duniani kuwa maisha ya utajiri na heshima na kwa uweza wako umenitukuza na kuniwezesha katika kila jambo maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Malango yako nayo yatakuwa wazi daima; Hayatafungwa mchana wala usiku; Ili watu wapate kukuletea utajiri wa mataifa, Na wafalme wao wakiongozwa pamoja nao"** ( Isaya 60:11 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Malango yangu yote ya maisha yako wazi daima hayatafungwa mchana wala usiku na watu wananiletea utajiri maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Mimi, niliye mdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwahubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika"** ( Waefeso 3:8 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Ndani ya Yesu Kristo kuna utajiri usiopimika ambao ni haki yangu kuwa nao asante Mungu Baba kunijaza na utajiri wa Yesu Kristo maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya**

**Kristo Yesu"** ( Wafilipi 4:19 ). Tamka kwa kinywa chako maneno haya kila siku kwamba **Mungu Baba umenijaza na kila kitu ninachokihitaji maishani mwangu umenipatia kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka"** ( Ufunuo wa Yohana 5:12 ). Tamka kwa kinywa chako maneno haya kila siku kwamba **Mimi nimemwamini na kumkiri na kumpokea Bwana Yesu maishani mwangu hivyo kupitia Yesu Kristo nimepokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka maishani mwangu kila siku kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake"** ( 2 Wakorintho 8:9 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Bwana Yesu alifanyika maskini ili mimi niwe**

**tajiri natangaza hapa duniani nitayaishi maisha ya utajiri na mafanikio siku zangu zote kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa"** ( Zaburi 1:3 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Maisha yangu ni sawa na mti uliopo kwenye vijito vya maji ambayo yanazaa matunda kwa majira yake na kila nilitendalo maishani mwangu litafanikiwa kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Biblia inasema kwamba **"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na**

**kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi"** ( Mwanzo 1:26-28 ). Tamka kwa kinywa chako kila siku maneno haya kwamba **Kwa kuwa Mungu amenifanya kwa mfano na sura yake mimi nitaishi hapa duniani maisha ya kutawala na kumiliki nitaishi maisha ya baraka na maisha ya kuzaa na kuongezeka kila siku kwa Jina la Yesu Kristo Amen**.

Hakikisha kila siku unatumia kinywa chako kutamka maneno ya baraka kuhusiana na maisha yako ya kila siku hakuna haja ukatumia kinywa chako kutamka maneno ya laana eti kwasababu ya mahali unapopitia pangumu kimaisha hapana ndio maana nimekuonyesha baadhi ya hiyo mistari ya Neno la Mungu unayotakiwa kuikiri kwa kinywa chako kila siku naamini kwamba Roho Mtakatifu atakuongoza na mistari mingine iliyomo ndani ya Biblia.

## ( 2 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Ushindi wako wa maisha.

Ulimwengu wako wa roho wa maisha unahusika sana na ushindi wako kwahiyo kiwango chako cha ushindi kwenye kila eneo la maisha yako kitatokana na hali ya utendaji kazi wa ulimwengu wako wa roho, hivyo unapokuwa unatumia kinywa chako kuongea maneno ya kushindwa au maneno ya uovu yasiyofaa unasababisha ulimwengu wako wa roho usiachilie viwango vikubwa vya ushindi maishani mwako ndio maana unatakiwa kila siku utumie kinywa chako kuongea maneno mazuri ya ushindi bila kuangalia vita au hali unazopitia kimaisha.

Biblia inasema kwamba **"Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda"** ( Warumi 8:37 ). Sisi ni washindi katika mambo yote sio katika mambo machache kwahiyo unatakiwa kutumia kinywa chako kutamka maneno haya kila siku kwamba **mimi ni mshindi katika mambo yote** kisha anza kutangaza ushindi kwenye kila eneo la maisha yako bila kutazama hali ya hilo eneo ikoje na kadiri

unavyotangaza ushindi ndivyo utakavyoona kila siku ushindi wa Mungu kwenye hilo eneo.

Ushindi wa maisha yako kwenye kila eneo hautokani na nguvu zako wewe bali unatokana na Mungu aliyekuumba na pia unatokana na wewe kuwa na Yesu Kristo na tena unatokana na wewe kuongozwa na Roho Mtakatifu maishani mwako.

Biblia inasema kwamba **"Kila mmoja aliyeitwa kwa jina langu, niliyemwumba kwa ajili ya utukufu wangu; mimi nimemwumba, naam, mimi nimemfanya"** ( Isaya 43:7 ). Mungu aliyekuumba yeye tabia yake ni tabia ya ushindi na kwasababu ndiye aliyekuumba na kukuleta hapa duniani maana yake Mungu anakusudia kukuona na wewe ukiishi katika maisha ya ushindi sio kushindwa ila makosa tunayofanya ni kutumia vinywa vyetu kutamka maneno ya kushindwa badala ya kutamka maneno ya ushindi, hakuna siku kwenye Biblia Mungu wala Yesu Kristo wala Roho Mtakatifu walitamka kushindwa bali siku zote wamekuwa wanatamka ushindi. Ndivyo na wewe katika maisha yako hapa duniani hakikisha unatumia kinywa chako kutamka maneno ya ushindi hata kama mazingira yanakuonyesha

kudhindwa bali wewe yaambie wazi hayo mazingira kwamba **Mimi nimeumbwa kushinda na mimi ni mshindi katika mambo yote kwa Jina la Yesu Kristo**.

Biblia inasema katika 2 Wakorintho 5:17 kwamba **"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya"** ( 2 Wakorintho 5:17 ). Tukiwa ndani ya Yesu Kristo sisi ni viumbe au watu wapya kwa maana kwamba sisi ni washindi kwahiyo kama umeokoka fahamu kwamba wewe ni Mtu mpya ndani ya Yesu Kristo na katika mfumo wa Wokovu wa Yesu Kristo hakuna kushindwa bali ni ushindi tu kwahiyo jitambue wazi kwamba wewe ni mshindi na tumia kinywa chako kutamka maneno ya ushindi kila siku na kwenye kila eneo la maisha yako.

Biblia inasema **"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia"** ( Yohana 14:26 ). Yesu Kristo alipokuwa anaondoka hapa duniani alisema kwamba atamtuma kwetu Roho Mtakatifu ili tusibakie peke

yetu na kati ya kazi alizonazo Roho Mtakatifu ni kutufundisha na kutukumbusha yote kwahiyo siku zote Roho Mtakatifu atakuwa anakukumbusha kwamba umeumbwa kushinda na atakufundisha njia mbalimbali za ushindi kwenye maeneo ya maisha yako kama utampatia nafasi, hivyo hakikisha kabla hujafanya jambo lolote lile mshirikishe Roho Mtakatifu na tena kama unataka Roho Mtakatifu afanye kazi nawe tumia kinywa chako kila siku kuongea maneno ya ushindi wala sio maneno ya kushindwa.

Kila siku ukiongea maneno ya ushindi unampatia nafasi Mungu na ufalme wake kukuhudumia na kutenda mambo makubwa maishani mwako lakini ukitumia kinywa chako kuongea maneno ya kushindwa unauzuia ufalme wa Mungu kukuhudumia kimaisha kila siku.

## ( 3 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Nafasi zako za maisha.

Kila Mtu anayo nafasi yake ambayo Mungu ameitengeneza kwenye ulimwengu wake wa roho na nafasi hizo za maisha yako zilizopo rohoni ndizo zinazokutengeneza kuwa mtu wa aina fulani hapa

duniani katika maisha yako, ndio maana kuna vitu kubwa sana kwenye maisha ya wanadamu kutoka kwenye nguvu za giza wakishambuliwa ili wasikae wala kutembea kwenye nafasi zao za maisha walizokusudiwa na Mungu maishani mwao. Biblia inasema kwamba **"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza"** ( Mwanzo 2:15 ) unamuona Mungu alimchukua Adamu kisha akamuweka kwenye bustani ya Edeni hivyo nafasi hiyo Mungu alimtengenezea Adamu kisha akamchukua mwenyewe na kumuweka kwenye hiyo nafasi ambayo ilikuwa imebeba mahitaji ya Adamu na ukuu wake hapa duniani.

Shetani alipoona Adamu amekaa kwenye nafasi yake na kupokea yale ambayo Mungu aliyakusudia kwake na Adamu kuishi maisha ya kusudi la Mungu kitu hicho hakikumfurahisha na alitafuta namna mbalimbali za kumtoa Adamu kwenye nafasi yake ya maisha na hatimaye alifanikiwa. Siku moja muda wa jioni Mungu alipomtembelea Adamu kwenye nafasi yake akamkuta hayupo ndio akamuuliza swali hili **"Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi?"** ( Mwanzo

3:9 ) swali hili uko wapi? Maana yake mbona Adamu sikuoni kwenye nafasi yako niliyokuweka? Hii vita hadi leo Shetani anaiendeleza ya kupambana na wanadamu na kuwatoa kwenye nafasi zao za kiroho za maisha walizokusudiwa na Mungu kukaa na kutembea na ukitolewa kwenye nafasi yako ya maisha rohoni unapoteza kila kitu kilochokuwa kinaambatana na hiyo nafasi.

Biblia inasema kwamba **"Akanitoa akanipeleka panapo nafasi; Aliniponya kwa kuwa alipendezwa nami"** ( 2 Samweli 22:20 ). Mungu anayo nafasi ya maisha ya kila mwanadamu anayemleta hapa duniani na kuzimu inayo vita ya kuhakikisha mwanadamu hakai kwenye nafasi yake aliyopangiwa na Mungu. Maneno unayoongea kupitia kinywa chako yanaweza kukuweka katika nafasi yako ya maisha au kukuondoa kwenye nafasi yako ya maisha hivyo chunga sana maneno yako na hakikisha kila siku unaongea maneno yenye Utukufu wa Mungu ili Mungu azidi kukuketisha kwenye nafasi yako lakini ukitumia kinywa chako kuongea maneno ya uovu naya upuuzi Shetani na kuzimu watashindana nawe

utoke kwenye nafasi yako ya maisha sababu watayatumia hayo hayo maneno yako.

## ( 4 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Watu walio na msaada wako wa maisha.

Ulimwengu wako wa roho ndio uliobeba na kuhusika na watu walio na msaada wa maisha yako ambao unatakiwa kukutana nao kila wakati ili wakusaidie kutoka hatua moja ya kimaisha na kwenda hatua nyingine ya kimaisha pia wakusaidie kukufikisha kwenye ndoto zako au hatima yako ya maisha. Kumbuka kwamba Mungu anawatumia watu kwaajili ya maisha yako kwa sababu chochote unachokihitaji maishani mwako Mungu amekiweka ndani ya mtu hivyo anavyofanya unapomuomba anakuunganisha na huyo mtu ili kijibu ombi lako ulilolipeleka mbele zake.

Biblia inasema hivi **"Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda; kwa sababu hiyo nitatoa watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwa ajili ya maisha yako"** ( Isaya 43:4 ). Mungu anatoa watu kwaajili yako na kabila za watu kwaajili ya maisha yako kwahiyo

Mungu aliyekuumba na kukuleta hapa duniani anao watu kwaajili ya maisha yako, ila unaweza kumzuia Mungu asikukutanishe na hao watu sahihi wa maisha yako kutokana na matumizi mabaya ya kinywa chako kwa maneno unayojitamkia na kuyaongea kuhusu maisha yako.

Biblia inatuambia kwamba **"Maana siku kwa siku humjia Daudi watu wa kumsaidia, hata wakapata kuwa jeshi kubwa, kama jeshi la Mungu"** ( 1 Mambo ya Nyakati 12:22 ). Siku kwa siku Mungu alihakikisha watu wanamjia Daudi kwenye maisha yake wa kumsaidia kumbe kama tutaongea maneno mazuri kila siku anayotupa Mungu kuishi atatuunganisha na watu wa msaada wetu kwa njia zake yeye, hivyo nakusihi sana kwamba hakikisha kila siku kwenye kinywa chako unaongea maneno mazuri na yenye utukufu wa Mungu na kukiri mistari mbalimbali ya Biblia na utamuona Mungu akikuunganisha na watu sahihi walio msaada wa hatima yako hapa duniani.

## ( 5 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Kusudi lako la Uumbaji.

Ulimwengu wako wa roho ndio unaohusika kwa asilimia zote na Kusudi la Mungu la uumbaji wako hapa duniani fahamu kwamba kila Mtu ameumbwa na Mungu kwa kusudi lake maalum na kila mwanadamu ambaye Mungu ameruhusu azaliwe hapa duniani amemleta ili aweze kulitumikia kusudi la Mungu siku zake zote za maisha yake. Biblia inasema hivi **"Bwana amefanya kila kitu kwa kusudi lake; Naam, hata wabaya kwa siku ya ubaya"** ( Mithali 16:4 ) Mungu amefanya kila kitu akiwepo wewe kwa kusudi lake hivyo wewe ni matokeo ya kusudi la Mungu na umeletwa hapa duniani kulitumikia kusudi la Mungu peke yake sio kutumikia kusudi la Shetani na ulimwengu huu hapana.

Biblia inasema kwamba **"Kwa maana Daudi, akiisha kulitumikia shauri/Kusudi la Mungu katika kizazi chake, alilala, akawekwa pamoja na baba zake, akaona uharibifu"** ( Matendo ya Mitume 13:36 ). Daudi katika maisha yake hakutumikia kusudi la wazazi wake wala kusudi la Shetani wala kusudi la wanadamu bali

alilitumikia kusudi la Mungu na alipolimaliza akalala maana yake akafariki. Mimi na wewe Mungu ametuleta hapa duniani ili tulitumikia kusudi lake la uumbaji kwa kipindi cha kuishi kwetu kwahiyo hakikisha unalitambua kusudi la Mungu juu yako na ulitumikie na kuliishi siku zako zote na kulikamilisha kabla hujatoka ndani ya huo mwili wako na kurudi mbinguni.

Unaweza kulifunga na kuzuia Kusudi la Mungu maishani mwako lisitende kazi na kufunuliwa kwako kwa sababu ya maneno unayoongea kila siku, chunga sana matumizi yako ya kinywa sababu kuna maneno unaweza kuyaongea na yakatumika na maadui wa kuzimu kulifunga au kulipindisha kusudi lako la maisha hivyo hakikisha unaongea maneno mazuri yaliyojengwa kwenye msingi wa Neno la Mungu kuhusu maisha yako ya kila siku hapa duniani.

## ( 6 ) Ulimwengu wako wa roho unahusika na Hatua zako za kimaisha.

Ulimwengu wako wa roho unahusika sana na hatua zako za maisha hapa duniani kwa sababu kila mwanadamu anazo hatua zake za maisha ambazo

haziwezi kulingana na mwanadamu mwingine. Biblia inasema **"Hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, Naye aipenda njia yake"** ( Zaburi 37:23 ) Unazo hatua zako za maisha ambazo zinatakiwa kuimarishwa na Mungu ila kwa maneno yako ya upuuzi na maovu unayoongea kila siku yanaweza kumzuia Mungu asiziimarishe hatua zako za maisha hapa duniani. Unapoishi kwa kulikiri Neno la Mungu kwa kinuwa chako kila siku Mungu atahusika kuziongoza na kuziimarisha hatua zako za maisha ili ufike mahali alipokupangia kimaisha alipokuleta hapa duniani, usikubali kuzifunga hatua zako za maisha kwa maneno yako unayoongea na kujitamkia kuhusiana na maisha yako ya kila siku.

● Naamini kwamba umefahamu na kuelewa sana kwa undani kuhusiana na eneo hili la kwanza la maisha yako ambalo ni ulimwengu wako wa roho nimekuchambulia vitu hivyo vichache vinavyohusika na ulimwengu wako wa roho wa maisha kwahiyo chunga sana maneno unayoongea kila siku ya maisha yako kwa sababu kila neno unaloongea unaliandika kwenye ulimwengu wa roho wa maisha yako natamani kila siku Mungu anayokupatia uweze kutumia kinywa chako

kuandika maneno mazuri yaliyo na Utukufu kwa Mungu kwenye ulimwengu wako wa roho wa maisha na kupitia hayo maneno yenye utukufu utamuona Mungu akisimama nawe na kujifunua kwako na kukutendea mambo makubwa kila siku ya maisha yako.

Naomba kiri maombi haya **"Mungu Baba naomba unisamehe mimi kwa sababu nimekitumia kinywa changu ulichonipa kuongea na kujitamkia maneno maovu na maneno yasiyofaa yaliyo na upumbavu na ujinga ninatubu kwako kwa Damu ya Yesu Kristo naomba unisamehe kabisa na kunitakasa nami nafuta maneno yote yasiyofaa na maneno yote ya uovu niliyoyaandika kwenye ulimwengu wangu wa roho ninayafuta kwa Damu ya Yesu Kristo na kuyaondoa kwa Jina la Yesu Kristo natangaza hayasimama hayo maneno na kutenda kazi maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo. Roho Mtakatifu naomba tawala lango la kinywa changu na kunisaidia ili niweze kutumia kinywa changu kila siku kuongea maneno yenye utukufu wa Mungu**

**kwaajili ya maisha yangu katika Jina la Yesu Kristo nimeomba na kuamini Amen"**. Kwa kukiri maombi haya Mungu ameshakusamehe hivyo usirudie tena kutumia kinywa chako kuongea maneno ya uovu bali tumia kinywa chako kila siku kuongea maneno mazuri na maneno ya ushindi na maneno yenye utukufu kwa Mungu.

---

ENEO LA PILI:

**Kila neno unaloongea unaliandika kwenye ulimwengu wa roho wa mbingu zako za maisha**.

---

Fahamu kwamba eneo lingine ambalo unaandika maneno unayoongea kila siku kwenye kinywa chako ni eneo la mbingu zako za maisha nataka ujue wazi kwamba kila neno unaloongea kwenye kinywa chako unaliandika katika mbingu zako za maisha na hayo maneno unayoyaandika kwenye mbingu zako za maisha ndio yatakayoamua hali ya utendaji kazi wa mbingu zako kila siku hapa duniani. Kila mwanadamu anazo mbingu zake za maisha ambazo zinahusika na maisha yake ya kila

siku hapa duniani, Biblia inasema hivi **"Na mbingu zako zilizo juu ya kichwa chako zitakuwa shaba, na nchi iliyo chini yako itakuwa chuma"** ( Kumbukumbu la Torati 28:23 ) Biblia haisemi na mbingu zetu bali inasema na mbingu zako kwa maana kwamba kila Mtu anazo mbingu zake za maisha zinazohusika na kuamua aina ya maisha atakayoyaishi hapa duniani. Hebu fikiria mbingu zako zilizo juu ya kichwa chako zikiwa shaba unafikiri utaishi maisha ya aiga gani? Maana yake utaishi maisha magumu naya kuteseka sana.

Wakati Mungu alipokuwa anaumba mbingu alitamka neno la kinywa chake tu **"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi"** ( Mwanzo 1:1 ). Mbingu na nchi zilitokana na neno ambalo Mungu alitamka kwa kinywa chake, kwahiyo kuna mahusiano makubwa sana ya utendaji kazi wa mbingu na maneno hivyo fahamu kuwa maneno unayoongea kwenye kinywa chako unayaandika kwenye mbingu zako nayo yatahusika na mbingu zako kila siku kwahiyo ukiongea maneno mazuri unafanya mbingu zako ziwe wazi na zifanye kazi vizuri kwenye maisha yako lakini ukiongea maneno machafu naya uovu unasababisha mbingu zako

kufunga nawe utaishi maisha magumu naya kuteseka na kuhangaika hapa duniani.

Biblia inasema **"Hivyo ndivyo vizazi vya mbingu na nchi zilipoumbwa. Siku ile Bwana Mungu alipoziumba mbingu na nchi"** ( Mwanzo 2:4 ). Ukisoma huu mstari kwa jicho la kiroho unatufunulia kwamba kuna mahusiano ya mbingu na uzao wa mwanadamu ndio maana inasema vizazi vya mbingu na nchi kwahiyo kitu chochote kinachoendelea kwenye mbingu zako na ardhi kinagusa maisha yako na maisha ya uzao wako ndio maana unatakiwa kuchunga sana maneno ya kinywa chako kwa sababu unaweza kuyafunga maisha ya kizazi/uzao wako kwa maneno unayoyatamka wewe mzazi sababu yatakuwa kumbukumbu hayo maneno kwenye mbingu kwaajili ya maisha yako na uzao wako, hakikisha wewe mzazi kila siku unaongea maneno ya utukufu kwaajili ya uzao wako pia hata wewe ambaye sio mzazi hakikisha unaongea maneno ua utukufu ili kuyaandika kwenye mbingu zako na mbingu za uzao wako.

Biblia inasema **"Nazishuhudiza mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele**

**yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako"** ( Kumbukumbu la Torati 30:19 ). Fahamu kwamba mbingu na nchi zinatumika kama shahidi wa maisha yako, katika tafasiri ya Neno Biblia imeeleza vizuri kwamba **"Leo ninaziita mbingu na nchi kama mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na laana. Basi sasa chagueni uzima, ili wewe na watoto wako mpate kuishi"**. Hivyo kila neno unaloongea kila siku kwenye kinywa chako usisahau mbingu na nchi/ardhi wanashuhudia hayo maneno yako kwamba umeongea maneno yenye utukufu au umeongea maneno maovu kwahiyo unaweza kuyafunga maisha yako na kuzifunga mbingu zako za maisha kutokana na maneno ya kinywa chako unayojitamkia na kuyaongea kila siku chunga sana sana.

Biblia inasema kwamba **"Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitanena; Na nchi isikie maneno ya kinywa changu"** ( Kumbukumbu la Torati 32:1 ). Mbingu zinaambiwa zisikilize maneno yanayotamkwa na nchi/ ardhi isikilize nayo nilitaka

uone jambo hili wazi wazi kwamba mbingu zinasikiliza maneno ya kinywa chako unayoongea kila siku maishani mwako kwahiyo hakikisha unakitumia kinywa chako kila siku kuongea maneno ya utukufu ili mbingu zako ziandike mambo mema kwenye maisha yako na kuachilia mambo mema kwako wewe. Mzazi kila neno unalotamka kwa mtoto wako unaliandika kwenye mbingu zake za maisha hivyo hakikisha unawatamkia maneno ya utukufu watoto wako kila siku maishani mwao ili mbingu zao zitende kazi ya kuwapa mambo mema.

Biblia inasema kwamba **"Je! Unazijua amri zilizoamuriwa mbingu? Waweza kuyathibitisha mamlaka yake juu ya dunia?"** ( Ayubu 38:33 ). Mungu alipoumba na kutengeneza mbingu aliweka amri au sheria zake zinazoziongoza mbingu na kati ya kitu kimojawapo ambacho ni sheria katika mbingu kilichowekwa na Mungu ni mbingu kufuatilia maneno ya watu walioko chini yake kwahiyo maneno yote unayoongea ukiwa chini ya mbingu yanasikilizwa kwenye mbingu na kufanyiwa kazi hivyo siku zako zote tumia kinywa chako kuongea maneno mazuri yenye utukufu kwa

Mungu hakikisha unakiri mistari mbalimbali ya Neno la Mungu kila siku ili kuandika maneno yenye utukufu kwenye mbingu zako wala usijaribu kutumia kinywa chako kila siku kuongea maneno ya uovu yatakutesa sana maishani mwako.

Tafsiri ya Neno Biblia inasema kwamba **"Hata hivyo alitoa amri kwa anga zilizo juu na kufungua milango ya mbingu, akawanyeshea mana ili watu wale; aliwapa nafaka ya mbinguni. Watu walikula mkate wa malaika, akawatumia chakula chote ambacho wangeliweza kula"** ( Zaburi 78:23-25 ). Biblia inatuambia jambo la muhimu sana hapa kwamba kwenye mbingu kuna milango na Mungu aliwalisha wana wa Israeli mana baada ya kufungua milango ya mbingu kumbe kuna vitu maishani mwetu ili tuvipokee ni lazima milango ya mbingu zetu ifunguliwe. Maneno yako unayoongea kila siku kupitia kinywa chako yanaweza kufungua milango ya mbingu zako na ukapokea vitu vya thamani maishani mwako au yanaweza kuifunga milango ya mbingu zako na kuishi maisha magumu hivyo nakuomba sana kila siku ongea maneno mazuri yenye utukufu ili milango ya mbingu zako

ifunguliwe na kutumiwa na Mungu kwaajili ya kukupa vitu vya thamani maishani mwako.

Biblia inasema kwamba **"Akaomba tena, mbingu zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa matunda yake"** ( Yakobo 5:18 ). Mbingu zimewekewa uwezo wa kutoa vitu ambavyo vimefichwa ndani yake na Mungu kwahiyo ukiongea maneno yenye utukufu kila kitu chema katika mbingu itakupatia maishani mwako nawe utaishi kama Mungu alivyokukusudia hapa duniani alipokuleta.

Kiri Maombi haya **"Mungu Baba kwa Jina la Yesu Kristo ninaomba toba mbele zako kutokana na maneno ya kinywa changu ambayo nimekuwa nikiyatamka kuhusiana na maisha yangu ya kila siku hapa duniani ninatubu pia hata kwaajili ya mbingu zangu za maisha na mbingu za eneo ninaloishi na kufanyia kazi naomba rehema zako kwa Damu ya Yesu Kristo nami nazitakasa mbingu zangu za maisha kwa Damu ya Yesu Kristo na mbingu za mahali ninapoishi na kufanyia kazi nazitakasa kwa Damu ya Yesu Kristo. Na leo ninazifungua mbingu zangu za maisha kutoka kwenye maneno yote**

**niliyowahi kuyatamka maishani mwangu ya uovu na maneno mabaya ninayafuta na kuyaondoa kwenye mbingu zangu kwa Jina la Yesu na mbingu zangu zifunguke kwa Jina la Yesu Kristo nazo ziwe wazi na Roho wa Mungu tawala mbingu zangu na Mungu Baba zitumie mbingu zangu kutimiza mipango yako maishani mwangu hapa duniani katika Jina la Yesu Kristo ninaomba na kuamini Amen"**.

Hakikisha sasa kuanzia leo unatumia vizuri kinywa chako kuongea maneno yenye utukufu kwaajili ya maisha yako ya kila siku zikiri ahadi za Neno la Mungu maishani mwako kila siku.

---

ENEO LA TATU:

**Kila neno unaloongea unaliandika kwenye ulimwengu wa roho wa ardhi unayoishi juu yake**.

---

Nataka ufahamu kwamba maneno unayoongea kwa kinywa chako huwa unayaandika kwenye ardhi na ardhi itafanya kazi kwenye maisha yako

sawasawa na maneno yako iliyoyabeba na kama ardhi imebeba maneno ya laana maana yake itafanya kazi kwako kinyume na mapenzi ya Mungu na kujikuta unaishi maisha ya laana na kama ardhi imebeba maneno ya baraka maana yake itafanya kazi kwako sawasawa na mapenzi ya Mungu na kujikuta unaishi maisha mazuri ya baraka.

Unakumbuka kwamba mwili wa mwanadamu Mungu aliuumba au kuutengeneza kutokea kwenye udogo/ardhi hebu soma mstari huu **"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai"** ( Mwanzo 2:7 ). Hivyo kuna mahusiano makubwa sana kati ya maisha ya mwanadamu na ardhi kwasababu mwili wake umetokana na mavumbi ya ardhi. Biblia inasema hivi **"Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni. Kama alivyo yeye wa udongo, ndivyo walivyo walio wa udongo; na kama alivyo yeye wa mbinguni, ndivyo walivyo walio wa mbinguni. Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake**

**yeye aliye wa mbinguni"** ( 1 Wakorintho 15:47-49 ).

Akisema mtu aliyetoka mbinguni anazungumzia roho yako ambapo ni wewe lakini uko ndani ya nyumba inayoitwa mwili na akisema aliyetoka kwenye udongo anazungumzia kuhusu mwili wako, kwahiyo ufahamu wazi wazi kwamba kuna mahusiano makubwa sana ya kiroho katika ya maisha yako na ardhi ndio maana hutakiwi kuongeaongea maneno ya uovu sababu ardhi inayasikia na inaweza kusimama kinyume na maisha yako pia usiwe mtu wa kutenda vitu vya ujinga kinyume na Neno la Mungu maishani mwako.

Biblia inasema kwamba **"Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo"** ( Mwanzo 1:24 ). Mungu aliisemesha ardhi hebu tusome katika tafsiri ya Neno Biblia inasema hivi **"Mungu akasema, "Ardhi na itoe viumbe hai kulingana na aina zake: wanyama wa kufugwa, viumbe vitambaavyo ardhini na wanyama pori, kila mnyama kulingana na**

**aina yake" Ikawa hivyo"**. Ardhi iko na uwezo wa kusikia na umemuona Mungu alipeleka maneno yake kwenye ardhi na ardhi ikafanya sawasawa na maneno aliyoyatamka Mungu hii inatufundisha wazi kwamba aina ya maisha tunayoishi sasa hivi imetokana na maneno ambayo tumekuwa tunayaongea kwa vinywa vyetu na ardhi imefanya na inazidi kufanya sawasawa na maneno yetu tunayoongea ndio maana tunahitajika tuongee maneno ya baraka sio maneno ya laana na uovu maishani mwetu.

Biblia inasema kwamba **"Ee nchi, nchi, nchi, lisikie neno la Bwana. Bwana asema hivi, Andikeni habari za mtu huyu kwamba hana watoto, kwamba mtu huyu hatafanikiwa siku zake zote; maana hapana mtu katika wazao wake atakayefanikiwa, akiketi katika kiti cha enzi cha Daudi, na kutawala tena katika Yuda"** ( Yeremia 22:30 ). Katika tafsiri ya Neno Biblia inatuambia kwamba **"Ee nchi, nchi, nchi, sikia neno la Bwana! Hili ndilo Bwana asemalo: "Mwandike huyu mtu kama asiye na mtoto, mtu ambaye hatafanikiwa maisha yake yote, kwa maana hakuna mtoto wake**

**atakayefanikiwa, wala kukaa kwenye kiti cha enzi cha Daudi wala kuendelea kutawala katika Yuda"**. Ardhi inasemeshwa kwa maneno kwamba iandike habari za huyu mtu Konia kwamba hatafanikiwa yeye na uzao wake ninachotaka hapa uone ni kwamba ardhi inaweza kusimama kinyume cha mafanikio ya mwanadamu yeye na uzao wake hivyo unatakiwa kuchunga sana mwenendo wako na tabia zako kwasababu ardhi inaweza kusimama kinyume na mafanikio yako wewe na uzao wako usiishi tu unavyotaka kiholela holela hapana bali ishi sawasawa na kanuni za Neno la Mungu.

Biblia inasema kwamba **"Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani"** ( Mwanzo 4:10-12 ). Katika tafsiri ya Neno Biblia inasema kwamba **"Bwana akasema, "Umefanya nini? Sikiliza! Damu ya ndugu yako inanililia mimi kutoka ardhini. Sasa umelaaniwa na umehamishwa kutoka**

**ardhi, ambayo imefungua kinywa chake na kupokea damu ya ndugu yako kutoka mkononi mwako. Utakapoilima ardhi, haitakupa tena mazao yake. Utakuwa mtu wa kutangatanga duniani asiye na utulivu"**. Umeona ardhi inaweza kumtengenezea mwanadamu aina ya maisha ya kutangatanga na yasiyokuwa na utulivu hapa duniani kwahiyo ukiongea maneno ya laana na maneno ya uovu ma ukafanya vitu vilivyo kinyume na mapenzi ya Mungu unaweza kujikuta kwenye mfumo mbaya wa maisha uliotengenezewa na ardhi yaani kujikuta unaishi maisha ya kutangatanga na yasiyokuwa na utulivu wa kuzaliwa vitu vya thamani maishani mwako.

Biblia inasema kwamba **"Nyoka akatoa katika kinywa chake, nyuma ya huyo mwanamke, maji kama mto, amfanye kuchukuliwa na mto ule. Nchi ikamsaidia mwanamke; nchi ikafunua kinywa chake, ikaumeza mto ule alioutoa yule joka katika kinywa chake"** ( Ufunuo wa Yohana 12:15-16 ). Hapa unaiona nchi maana yake ardhi ikimsaidia huyu mwanamke asiangamizwe na mto wa mafuriko wa Shetani hii

inatupatia maana kwamba ardhi inaweza kusimama upande wako kukusaidia au ikasimama upande wako kukuangamiza. Unapotumia kinywa chako kuongea maneno ya baraka naya utukufu maana yake unaifanya ardhi isimame upande wako kila siku kukusaidia kimaisha na unapotumia kinywa chako kuongea maneno ya laana naya uovu maana yake unaifanya ardhi kisimama kinyume cha maisha yako na kukuangamiza na kukutesa.

Nakuomba sana mwana wa Mungu tumia kinywa chako kuongea kila siku maneno yenye utukufu na maneno ya baraka kuhusu maisha yako na kuhusu vitu vyako ili ardhi ikuzalie vitu vyema na mbingu za Mungu zitimize mipango yake maishani mwako, pia hakikisha unaishi sawasawa na kanuni zote za Neno la Mungu ukitambua wazi kwamba ardhi inafuatilia maneno yako unayoongea pia inafuatilia matendo na mwenendo wako wa kila siku.

Kiri Maombi haya kwa Imani **"Mungu Baba kwa Jina la Yesu Kristo ninaomba toba na rehema mbele zako kutokana na mimi kutumia kinywa changu vibaya na kuongea maneno yasiyofaa maneno ya laana na maneno ya**

**uovu kuhusu maisha yangu hapa duniani pia nisamehe na kunirehemu Mungu kutokana na mwenendo na tabia zangu zilizo kinyume na kanuni za Neno lako naomba rehema kwa Damu ya Yesu Kristo. Leo napita kwenye ulimwengu wa roho wa ardhi na kufuta maneno yote ya laana na maneno yote ya uovu yasiyofaa niliyoyatamka maishani mwangu na ardhi inayasikia na kuyatunza na kuyatendea kazi ninayafuta yote hayo maneno kwa Damu ya Yesu Kristo na kuyaondoa kwenye utendaji kazi wa ardhi kwa Jina la Yesu Kristo.**

**Nami leo najifungua kwenye vifungo vyote vya ardhi kwa Jina la Yesu Kristo na maisha yangu yaliyofungwa kwenye ardhi leo nayafungua kwa Jina la Yesu Kristo na kuyakomboa kwa Damu ya Yesu Kristo, ninakuamuru wewe ardhi kuanzia sasa utasimama upande wangu na kunitendea mema na kunizalia mazao mazuri maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo nami nakuamuru wewe ardhi utabeba baraka kwaajili ya maisha yangu wala hautabeba**

**laana kwaajili ya maisha yangu kwa Jina la Yesu Kristo nimeomba na kuamini Amen**.

Baada ya kuomba maombi haya Mungu amekusamehe uovu wa maneno yako hakikisha sasa unatumia kinywa chako kila siku kuongea maneno ya utukufu na maneno ya baraka bila kujalisha unapitia katika hali gani kimaisha na Mungu atazidi kukutendea mambo makubwa maishani mwako hapa duniani kila siku.

**USISAHAU MAMBO HAYA KUHUSU KINYWA CHAKO**:

Nataka nikukumbushe mambo haya usiyasahau ili uweze kuwa mwangalifu sana na maneno unayoongea kuhusu maisha yako kila siku;

**( A ) Kwa maneno ya kinywa chako unaweza kuijenga kesho yako iliyo bora au ukaiharibu kesho yako na ikawa mbaya**.

Mungu amekuandalia kesho ya maisha yako iliyo njema sana tena ya thamani alipokuleta hapa duniani ila unaweza kusababisha kwa maneno ya kinywa chako uwe na kesho njema au kwa maneno ya kinywa chako unaweza kuiharibu kesho yako na

kuishi kwenye mahangaiko na mateso mbalimbali kimaisha. Mungu alimwambia Musa kwamba **"Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengezea"** ( Kutoka 23:20 ), kuna mahali ambapo Mungu aliwatengenezea wana wa Israeli lakini walitakiwa kuwa waangalifu sana na mienendo yao wasije kumkasirisha yule Malaika wa Mungu aliyewatangulia hii inatupa picha kwamba ili tufike kwenye hatima zetu njema tulizoandaliwa na Mungu ni lazima tuchunge sana maneno yetu tunayoongea pia tuchunge mienendo yetu ya kila siku ya kimaisha.

Wana wa Israeli walishindwa kuingia nchi ya Kanaani kwasababu ya maneno ya vinywa vyao, angalia Biblia inasema **"Bwana akasema, Hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao; nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema, kisha pana; nchi ijaayo maziwa na**

**asali; hata mahali pa Mkanaani, na Mhiti, na Mwamori, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi"** ( Kutoka 3:7-8 ). Mungu aliwaahidi kabisa kwa kinywa chake wana wa Israeli kuwafikisha katika nchi ya Ahadi ya kanaani iliyojaa maziwa na asali baada ya kuwatoa nchi ya mateso ya Misri lakini walikuwa na maneno ya kunung'unika na kulalamika sana na kitendo hicho kilimchukiza sana Mungu.

Ukiwa na maneno ya kulalamika na kunung'unika unamchukiza sana Mungu **"Watu hawa ni wenye kunung'unika, wenye kulalamika, waendao kwa tamaa zao, na vinywa vyao vyanena maneno makuu mno ya kiburi, wakipendelea watu wenye cheo kwa ajili ya faida"** ( Yuda 1:16 ). Usikubali kuharibu kesho yako njema na kuiharibu hatima yako njema uliyopangiwa na Mungu kwa maneno ya kulalamika na kunung'unika kila siku hakikisha kinywa chako kinakuwa na maneno ya utukufu kwa Mungu hata kama unapitia wakati mgumu kimaisha chunga sana usiwe na kinywa cha maneno ya kulalamika na kunung'unika kumbuka kesho njema Mungu

atakufikisha na kukuingiza kwa Utukufu wake bila kujali mahali unapopitia leo hii.

**( B ) Kwa maneno ya kinywa chako unaweza kusababisha msaada wa Mungu uwe pamoja nawe muda wote au msaada wa Mungu ukae mbali nawe**.

Maneno unayoongea kila siku kwa kinywa chako yanaweza kusababisha msaada wa Mungu wa maisha yako kuwa pamoja nawe au msaada wa Mungu wa maisha yako uwe mbali nawe kwahiyo kama unataka kuuona msaada wa Mungu kila siku ya maisha yako hakikisha unaongea maneno ya utukufu na maneno mazuri na kuzikiri Ahadi za Mungu kila siku. Biblia inasema kwamba **"Maana Wewe umekuwa msaada wangu, Na uvulini mwa mbawa zako nitashangilia"** ( Zaburi 63:7 ), Mungu ndiye msaada wa maisha yetu hapa duniani naye anatamani sana kila siku atusaidie kwenye maisha yetu lakini maneno yetu tunayoongea kila siku kwa vinywa vyetu yanaweza kusababisha tupate msaada wake Mungu au tuukose msaada wake Mungu hivyo tuwe waangalifu sana na maneno yetu tunayoongea.

Biblia inasema kwamba **"Kwa msaada wa Mungu tutatenda makuu, Maana Yeye atawakanyaga watesi wetu"** ( Zaburi 108:13 ). Msaada wa Mungu ndio unaotuwezesha sisi kwenye maisha yetu tutende mambo makubwa ya kuishangaza hii dunia hivyo hakikisha kinywa chako kinaongea maneno ya utukufu ili msaada wa Mungu upatikane maishani mwako kila siku nawe utende mambo makubwa maishani mwako. Mungu anao msaada wake kwaajili ya ndoa yako na uchumi wako na elimu yako na familia yako na pia Mungu anao msaada kwaajili ya kazi zako na biashara zao n.k hivyo ongea maneno ya utukufu kwa kinywa chako na kila siku na utauona msaada wa Mungu wa viwango vya juu maishani mwako.

**( C ) Kwa maneno ya kinywa chako unaweza kuwaleta watu wazuri maishani mwako au ukawaleta watu wabaya na waovu maishani mwako**.

Kuna watu wako kwenye maisha yako ambao wamekuja kwasababu ya maneno yako unayojitamkia kila siku kuhusu maisha yako nataka utambue kwamba maneno yako yanaweza kuwaleta watu wazuri au kuwaleta watu wabaya

ndio maana mtu anaweza kutengeneza urafiki na mtu mwingine kutokana na vile anavyoongea kila wakati. Kwa mfano ukiongea maneno ya ovyo ovyo utawapata watu wa hovyo hovyo maishani mwako sababu watakupenda kwa kuwa unaongea kama wao maneno ya ovyo ovyo ila ukiongea maneno ya ushindi na maneno ya baraka utawapata watu wa baraka ambao watavutiwa nawe sababu unaongea kama wao pia wanavyoongea maneno ya baraka.

Biblia inasema **"Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako"** ( Danieli 10:12 ). Huyu ni Malaika anamwambia Danieli maneno yako yamenifanya nije kwako kwahiyo watu wa aina fulani watakuja kwenye maisha yako kutokana na aina ya maneno unayoongea kwa kinywa chako ukiwataka watu wazuri na watu wema ni lazima uongee maneno mazuri yenye utukufu kwa Mungu ila ukiwataka watu waovu na watu wa ovyo ovyo wewe ongea maneno mabaya na yasiyokuwa na maana.

Hata siku moja huwezi kuongea maneno ya utakatifu halafu watu wenye dhambi wakakaa karibu yako bali watu ambao ni watakatifu ndio watakaokaa karibu yako sababu mnaongea lugha moja ya maneno ni kama vile mlevi akimsikia mtu mwingine anaongea maneno ya ulevi levi anampenda na kukaa karibu naye sababu wanaendana lugha za maneno yao, Je! Wewe kwenye maisha yako unataka uzungukwe na watu wazuri au watu wabaya? Je! Unataka uzungukwe na watu watakatifu au wenye dhambi? Unataka uzungukwe na watu wa thamani au watu waovyo ovyo? Maamuzi yako kwako hakikisha unachunga sana maneno ya kinywa chako.

Biblia inatuambia kwamba **"Kwa kuwa ulikuwa wa thamani machoni pangu, na mwenye kuheshimiwa, nami nimekupenda; kwa sababu hiyo nitatoa watu kwa ajili yako; na kabila za watu kwa ajili ya maisha yako"** ( Isaya 43:4 ). Wewe kuwa wa thamani machoni pa Mungu ni wewe kuwa na maneno ya utukufu na ili uheshimike kwa Mungu na akupende anataka kukuona unaongea maneno yenye utukufu naye atatoa watu wazuri na watu wema kwaajili ya

maisha yako ambao watakuwa msaada kwako hivyo hivyo ukiwa mwenye kuongea maneno ya uovu Shetani atakupatia watu wa ovyo ovyo maishani mwako.

**( D ) Kwa maneno ya kinywa chako unaweza kuishi miaka mingi au ukaishi miaka mifupi**.

Maneno unayoongea kuhusu maisha yako yanaweza kukufanya uishi miaka mingi hapa duniani ile uliyopangiwa na Mungu au kwa maneno ya kinywa chako unaweza kufupisha siku zako za kuishi hapa duniani. Biblia inasema kwamba "Basi umetegwa kwa maneno ya kinywa chako, Umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako" ( Mithali 6:2 ) katika tafsiri ya Neno Biblia inasema **"kama umetegwa na ulichosema, umenaswa kwa maneno ya kinywa chako"**. Unachosema kwa kinywa chako kinaweza kukuacha uwe huru na kuishi miaka mingi au kukunasa na ukaishi maisha mafupi, unapokuwa unaongea maneno ya kufa kufa kila wakati maana yake unafupisha siku zako za kuishi hapa duniani lakini ukiongea maneno ya kuishi maisha marefu maana yake huwezi kufa mapema hapa duniani.

Biblia inasema kwamba **"Utafika kaburini mwenye umri mtimilifu, Kama mganda wa ngano ulivyo wakati wake"** ( Ayubu 5:26 ). Unaweza kufika kaburini ukiwa na umri mtimilifu maana yake umri uliokomaa kama utakuwa unaongea maneno ya kuishi miaka mingi ila unaweza kufika kaburi ukiwa na umri ambao haujakomaa kwasababu ya kuongea kila wakati maneno ya kufa kufa. Angalia mstari huu **"Tumbo la mtu litajazwa matunda ya kinywa chake; Atashiba mazao ya midomo yake. Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; Na wao waupendao watakula matunda yake"** ( Mithali 18:21 ) katika tafsiri ya Neno Biblia inatuambia **"Tumbo la mtu litajaa kutokana na tunda la kinywa chake, atashibishwa mavuno yanayotokana na midomo yake. Mauti na uzima viko katika uwezo wa ulimi, nao waupendao watakula matunda yake"**. Kwenye maneno yako unaweza kutoa uzima au mauti na kama utatoa maneno ya uzima utaishi miaka mingi uliyopangiwa na Mungu na kama utatoa mauti utaishi miaka michache bila kuifikia miaka ya utimilifu wako.

Kwahiyo hata kama umekata tamaa kutokana na hali mbalimbali unazopitia kimaisha hakikisha unaongea maneno ya uzima usijaribu kuongea maneno ya mauti yatakughalimu sana kiroho na kimwili. Mungu anatamani uishi miaka mingi hapa duniani **".... na hesabu ya siku zako nitaitimiza"** ( Kutoka 23:26 ) katika tafasiri ya Neno Biblia inasema **"....Nami nitakupa maisha makamilifu**". Hayo ndiyo mapenzi ya Mungu uwe na maisha makamilifu na uishi kwa miaka yote aliyokupangia sababu uko na Kusudi lake hapa duniani hakikisha unaongea maneno yenye utukufu na kuzikiri Ahadi za Mungu za maisha marefu zilizomo ndani ya Neno lake ( Biblia ).

## JE! MAISHANI MWAKO UMEMRUHUSU MUNGU AU SHETANI KUTUMIA KINYWA CHAKO?.

Ninapomalizia Darasa hili katika somo hili nataka nikuulize je! Umekubali kumruhusu nani atumie kinywa chako kila siku hapa duniani Mungu au Shetani? Hakikisha unamruhusu Mungu ndiye akitumie kinywa chako kila siku. Biblia inasema

kwamba **"Ee Bwana, uweke mlinzi kinywani pangu, Mngojezi mlangoni pa midomo yangu"** ( Zaburi 141:3 ) huyu ni Mtumishi wa Mungu Daudi alimuomba Mungu aweke mlinzi kinywani mwake ili asiongee maneno ya uovu bali aongee maneno ya utukufu kila siku nawe omba haya maombi ukiwa umeshika kinywa chako kwamba Mungu niwekee mlinzi katika kinywa changu ili niongee maneno ya utukufu kila siku hapa duniani.

### ( i ) Mungu aliye hai katika Yesu Kristo anaweza kukitumia kinywa cha mwanadamu.

Fahamu kwamba Mungu anaweza kabisa kukitumia kinywa cha mwanadamu na ndivyo anavyotamani kwamba kila siku akitumie kinywa cha kila mtu aliyemuumba na kumleta hapa duniani. Biblia inasema kwamba **"Kila mmoja aliyeitwa kwa jina langu, niliyemwumba kwa ajili ya utukufu wangu; mimi nimemwumba, naam, mimi nimemfanya"** ( Isaya 43:7 ) kwasababu Mungu ndiye aliyekuumba katika utukufu wake anatamani kinywa chako kiwe sehemu ya utukufu wake kwa kuongea maneno mazuri na maneno ya utukufu, huwaga Mungu anaumia sana moyoni

mwake kumuona mwanadamu aliyemuumba akitumia kinywa chake kuongea maneno ya uovu na maneno ya ovyo ovyo ni jambo linalomhuzunisha Mungu.

Biblia inasema kwamba **"Bwana akamwambia, Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu? Au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kuwa kipofu? Si mimi, Bwana?"** ( Kutoka 4:11 ). Ni Mungu alimuuliza swali hili Musa kwamba ni nani aliyekifanywa kinywa cha mwanadamu? Ni yeye Mungu hivyo Mungu anatarajia na kufurahi kuona kila kinywa cha mwanadamu alichokifanya kinatumika kumtukuza yeye na kumsifu yeye na kumshangilia yeye. Usijaribu kabisa kutumia kinywa chako kumtukuza Shetani wala wachawi wala waganga wa kienyeji wala mapepo wala usijaribu kutumia kinywa chako kumsifu Shetani wala kutumia kinywa chako kuimba nyimbo za ovyo ovyo za kidunia ambazo hazina utukufu kwa Mungu, hakikisha kinywa chako kinampatia utukufu Mungu peke yake.

Biblia inasema **"Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta**

**haikuisha, sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa kinywa cha Eliya"** ( 1 Wafalme 17:16 ). Mungu alikitumia kinywa cha Nabii Eliya kwaajili ya maisha ya mama wa Serepta kumbe ni kiu ya Mungu atumie vinywa vyetu hapa duniani kubali kumruhusu Mungu akitumie kinywa chako kwaajili ya utukufu wake hapa duniani kila siku.

Biblia inasema kwamba **"Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana; Wote wenye mwili na walihimidi jina lake takatifu milele na milele"** ( Zaburi 145:21 ). Mungu anatamani kukiona kinywa chako kikinena sifa zake kila siku hivyo hakikisha unakitumia kinywa chako kutoa maneno ya kuzinena sifa za Mungu na kunena matendo makuu ya Mungu na kuzinena shuhuda za Mungu kila siku.

Biblia inasema kwamba **"Fadhili za Bwana nitaziimba milele; Kwa kinywa changu nitavijulisha vizazi vyote uaminifu wako"** ( Zaburi 89:1 ). Mungu anatamani kukiona kinywa chako kikitumika kuelezea kizazi chako na vizazi vijazo uaminifu wake na yale aliyokutendea wewe na kuelezea kizazi chako yale ambayo Mungu ana uweza na nguvu na mamlaka ya kuyatenda

kwenye maisha ya wanadamu. Hakikisha kizazi chako kinapokea maneno yenye utukufu kutoka kinywani mwako sio kupokea maneno ya kulalamika na kunung'unika hapana.

Biblia inasema **"Basi nikafunua kinywa changu, naye akanilisha lile gombo"** ( Ezekieli 3:2 ). Ezekieli alipokifunua kinywa chake Mungu akamlisha lile gombo ambalo ni Neno lake hii iko na maana kwamba Mungu anataka kuona kila wakati tukifunua vivywa vyetu tutoe Neno lake sio maneno ya uovu, hakikisha kinywa chako kinakuwa ni madhabahu ya Mungu ya kutoa Neno lake kila siku na kila wakati bali usikubali kinywa chako kiwe ni madhabahu ya uovu kwa kutoa maneno ya ovyo ovyo.

Kiri Maombi haya **"Mungu Baba kwa Jina la Yesu Kristo ninaomba toba na reheme mbele zako kutokana na mimi kukitumia kinywa changu kuwa madhabahu ya uovu leo ninaomba Damu ya Yesu Kristo ikitakase kinywa changu na kinywa changu nakiweka wakfu kwenye madhabahu yako Mungu nakuomba uniwekee mlinzi katika kinywa changu ili niongee maneno ya utukufu**

**maishani mwangu kwa Jina la Yesu Kristo. Leo nakubali kwa moyo wangu kukuruhusu Mungu Baba kukitumia kinywa changu kwaajili ya Ufalme wako na kwaajili ya utukufu wako kama ulivyotumia vinywa vya watumishi wako mbalimbali katika Biblia leo nakuomba Mungu kitumie kinywa changu siku zote za mimi kuishi hapa duniani na Roho Mtakatifu kiongoze kinywa changu kiongee kila siku maneno ya Utukufu na kulikiri Neno la Mungu kwa Jina la Yesu Kristo ninaomba na kuamini Amen"**.

Kwa maombi haya uliyoyaomba kwa Imani Mungu amekusikia na kinywa chako sasa kitatumika kwaajili ya Utukufu wa Mungu.

● Ukimruhusu Mungu akitumie kinywa chako maana yake utawaona Malaika wa Mungu wakihusika kukuhudumia maishani mwako kila siku **"Je, malaika wote si roho watumikao, waliotumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu?"** ( Waebrania 1:14 ). Siku zote kinywa chako kikitumiwa na Mungu utauona utendaji kazi wa malaika wa Mungu wakikuhudumia kwenye maisha yako kwenye kila

eneo na kila neno la utukufu nala baraka utakaloongea kwa kinywa chako utawaona malaika wa Mungu wakiyatimiza maisha mwako, nakuomba sana sana kwa kipindi hiki cha wewe kuishi hapa duniani mruhusu Mungu akitumie kinywa chako pia hakikisha kila siku unatumia kinywa chako kuongea maneno ya baraka na utukufu kuhusu maisha yako na kuhusu familia na uzao wako na kuhusu wanadamu wanaokuzunguka.

### ( ii ) Shetani anaweza kukitumia kinywa cha mwanadamu.

Fahamu kwamba Shetani anaweza kabisa kukitumia kinywa cha mwanadamu ili kiweze kuongea maneno ya uovu na jambo hili Mungu hapendi kuliona kwako wewe usikubali kabisa kuruhusu kinywa chako ulichopewa na Mungu alitumie shetani hapa duniani. Hebu tutafakari mistari hii ifuatayo tuone namna ambavyo Shetani anatumia vinywa vya wanadamu kila siku hapa duniani;

Biblia inasema **"Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru. Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi**

**arobaini na miwili"** ( Ufunuo wa Yohana 13:5 ). Shetani anaweza kutumia kinywa cha mwanadamu kiongee maneno ya makufuru hivyo usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kuongea maneno ya makufuru ambayo ni maneno ya uovu yasiyokuwa na heshima kwa Mungu.

Biblia inasema **"Kinywa cha mpumbavu ni uharibifu wake, Na midomo yake ni mtego wa nafsi yake"** ( Mithali 18:7 ). Shetani anaweza kukigeuza kinywa kizuri cha mwanadamu na kukifanya kiwe kinywa cha mpumbavu yaani kiongee maneno ya upumbavu tu nakuomba usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kuwa kama cha mpumbavu kwa kuongea maneno ya upumbavu na ujinga usikubali kabisa hilo bali kinywa chako kinatakiwa kuwa kinywa cha hekima na heshima kwa kuongea maneno mazuri.

Biblia inasema **"Maana kinywa changu kitasema kweli, Na uovu ni chukizo kwa midomo yangu"** ( Mithali 8:7 ). Shetani anatamani kutumia kinywa cha mwanadamu kuongea uongo kila siku kwahiyo usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kuongea maneno ya uongo bali kubali kinywa chako kiwe cha

kuongea kweli yaani kiwe kinachotoa maneno ya ukweli tu sio uongo.

Biblia inasema kwamba **"Umekiachia kinywa chako kinene mabaya, Na ulimi wako watunga hila"** ( Zaburi 50:19 ). Shetani anatamani sana kutumia kinywa cha mwanadamu kiongee maneno mabaya kwaajili ya maisha yake na kwaajili ya wanadamu wengine usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kuongea maneno mabaya kujihusu wewe mwenyewe au kuhusu wanadamu wengine bali kubali kinywa chako kiongee maneno mazuri kujihusu wewe na kuhusu wanadamu wanaokuzunguka.

Biblia inasema kwamba **"Kinywa chake kimejaa laana, Na hila na dhuluma. Chini ya ulimi wake kuna madhara na uovu"** ( Zaburi 10:7 ). Shetani anapenda sana kutumia kinywa cha mwanadamu kuongea maneno ya laana yaani mwanadamu ayalaani maisha yake mwenyewe na kulaani maisha ya watu wanaomzunguka usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kutoa maneno ya laana bali kitumie kinywa chako kuongea maneno ya Baraka kwaajili ya maisha

yako na kwaajili ya maisha ya watu wanaokuzunguka.

Biblia inasema kwamba **"Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu"** ( Wakolosai 3:8 ). Tena Biblia inasema **"Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia"** ( Waefeso 4:29 ). Shetani anatamani sana kutumia kinywa cha mwanadamu kuongea maneno ya uovu na kuongea matusi na maneno mengi sana yasiyomtukuza Mungu nakuomba sana usikubali kabisa Shetani akitumie kinywa chako kuongea matusi wala usikubali shetani akitumie kinywa chako kugombana na watu wala usikubali shetani akitumie kinywa chako kuongea maneno ya uovu bali kubali kinywa chako kiongee maneno ya utukufu na kinywa chako kiongee maneno ya baraka na ushindi kila siku.

● Ukimruhusu Shetani akitumie kinywa chako maana yake mapepo yake yatafanya kituo chao kwenye kinywa chako na jambo hili la kumruhusu Shetani kutumia kinywa chako litakuangamiza

kabisa wewe na uzao wako hapa duniani. Usikubali kabisa Shetani na mapepo ya kuzimu kutumia kinywa chako hata mara moja na muda wowote ukigundua kwamba mapepo yamekitumia kinywa chako kuongea maneno ya uovu na maneno ya ovyo ovyo fanya haraka kuingia kwenye maombi ya toba kwa Mungu kisha kuomba Damu ya Yesu kutakasa kinywa chako.

Kiri Maombi haya **"Katika Jina la Yesu Kristo Shetani na mapepo yako ya kuzimu nawatangazia kwamba hamtakitumia kinywa changu kwa namna yoyote ile kuongea maneno ya uovu na maneno ya matusi na magombana wala hamtakitumia kinywa changu kuongea maneno la kulaani wala maneno ya kulalamika na kunung'unika wala hamtakitumia kinywa changu kutukuza dhambi na uovu na nyimbo zako za kuzimu kwa Jina la Yesu Kristo leo nimeivunja nguvu yako Shetani na mapepo kwenye kinywa changu na leo nimekubali Mungu Baba aliyeniumba peke yake ndiye atakayekitumia kinywa changu na Roho Mtakatifu ili kuongea maneno ya utukufu na maneno ya**

**baraka na ushindi na kumsifu na kumtukuza yeye na kueleza matendo yake kwa Jina la Yesu Kristo nimeomba na kuamini Amen"**.

Hakika natambua wazi kwamba umebarikiwa sana kwa viwango vya juu kupitia Somo hili Ndani ya Darasa letu hili la Kupata Maarifa ya Kiroho, ni matumaini yangu utayafanyia kazi kila siku mambo yote uliyojifunza ndani ya kitabu hiki maishani mwako.

Biblia inasema kwamba "Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote" ( Wagalatia 6:6 ) katika tafsiri ya Neno Biblia inasema hivi **"Basi, yeye afundishwaye katika neno na amshirikishe mwalimu wake mema yote"**. Mwanafunzi anayefundishwa Neno la Mungu na akajengwa na kuimarishwa na kupokea Maarifa ya Ufahamu wa kiroho kupitia Neno la Mungu anatakiwa kumshirikisha mambo mema mwalimu wake huyo aliyejitoa kumfundisha na kumjenga kiroho. Pia Biblia inasema wazi katika tafsiri ya Neno Biblia kwamba **"Je, ikiwa sisi tulipanda mbegu ya kiroho miongoni mwenu, itakuwa ni jambo kubwa iwapo tutavuna vitu vya mwili kutoka kwenu?"** ( 1 Wakorintho

9:11 ). Mtumishi wa Mungu yeye anakupandia mbegu za kiroho za Neno la Mungu hivyo anatakiwa awe na sehemu ya ushirika katika baraka ulizonazo za maishani mwako.

Kwahiyo kama ambavyo umebarikiwa na Neno la Mungu katika somo hili nawe unaweza kufanyika baraka kwa Mungu katika Utumishi na huduma hii kupitia Sadaka zako na mali zako ili tuzidi kueneza habari njema za Ufalme wa Mungu, kwahiyo tumia number hii ya Utumishi **+255 765 867574 ( M-PESA )** kuwa chombo chako kutoa Sadaka zako kwa Mungu katika huduma hii ya Mungu ninayoifanya kila siku hapa duniani, na Mungu Baba akubariki zaidi na kukuzidishia maishani mwako na kuyajibu mahitaji yote ya moyoni mwako kwa Jina la Yesu Kristo. Kama utahitaji kutoa Sadaka zako kwa njia ya Benk wasiliana nami kwa number hiyo kisha utapewa Account ya Benk unayotumia.

Mimi ni Mwalimu wa Neno la Mungu la Maarifa

**Samwel Kibiriti**.

**@February 2024**.

Katika mitandao ya Facebook utayapata masomo yangu mbalimbali ninayofundisha kupitia Page hii ( **Mwlm Samwel Kibiriti Tanzania** au **Samwel Kibiriti ministry** ) na kama unahitaji kuyapata masomo ninayofundisha kwa njia ya AUDIO VOICE yaani kwa Sauti tunalo Group la Telegram wasiliana nami kwa hiyo number ya simu kwa kunitumia Ujumbe Inbox ya Talegramu nawe utaunganishwa pia tunayo magroup ya WhatsApp ambayo utayapata masomo ninayofundisha wewe wasiliana nami useme unataka tukuunganishe eneo lipi, yapo masomo mazuri yaliyobeba Maarifa ya Neno la Mungu ambayo yatakujenga na kukuinua zaidi kiroho na kiimani na kimaisha.

Mkono wa Mungu uzidi kukutendea mema na kukuinua Juu kimaisha na kiuchumi kila siku hapa duniani.